JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

05 Barabara ya Ikulu,
S. L. P. 275,
50101 KAWAJENSE
MPANDA CBD, KATAVI
BaruaPepe:
rbckatavi@pccb.go.tz.
Tovuti:
www.pccb.go.tz

KATAVI – 15 AGOSTI, 2023

TAKUKURU MKOA WA KATAVI YASHUGHULIKIA WAZABUNI WANAOSABABISHA KUCHELEWA UKAMILISHWAJI WA MIRADI YA MAENDELEO.

Taasisi ya kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Katavi imeendelea na utekelezaji wa majukumu yake katika robo ya Aprili hadi Juni, 2023 ambapo mkazo uliwekwa katika elimu ya kuhamasisha wananchi ili washiriki kikamilifu Kuzuia Rushwa na ufuatiliaji wa fedha za miradi ya maendeleo zilizotolewa na Serikali ikiwa ni pamoja na kufanyia kazi maelekezo yanayotolewa na viongozi wa nchi. Ofisi ya TAKUKURU, kwa kushirikiana na wananchi na wadau mbalimbali imefanikiwa kuwabaini wazabuni wanaosababisha ucheleweshwaji wa ukamilishwaji wa mradi wa kituo cha afya Ugalla wenye thamani ya **shilingi milioni 627**. Aidha, wazabuni hao wamekuwa wakikiuka taratibu za manunuzi ikiwa ni pamoja na kutowasilisha vifaa vya ujenzi wa kituo hicho licha ya kulipwa fedha kwa wakati kwa ajili ya vifaa hivyo. TAKUKURU mkoa wa Katavi inafanya uchunguzi dhidi ya wazabuni hao na pindi uchunguzi utakapokamilika hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao, ili iwe fundisho kwa wazabuni wengine wanajihusisha na ukiukwaji wa taratibu za manunuzi kwenye miradi ya maendeleo.

1. UZUIAJI RUSHWA

TAKUKURU mkoa wa Katavi imefuatilia utekelezaji wa miradi **11** yenye thamani ya **shilingi bilioni 2.83 (2,831,493,083/=)** katika sekta za barabara, elimu na afya. Aidha miradi **(2)** imekamilika, mradi **(1)** unaendelea vizuri na miradi **(8)** inaendelea kufuatiliwa kwa ukaribu kutokana mapungufu mbalimbali ikiwemo ucheleweshwaji na ubora wa miradi hiyo. **(KIAMBATANISHO 1)**

2. UCHAMBUZI

TAKUKURU imefanya, chambuzi za mifumo ikiwa na lengo la kubaini mianya ya Rushwa ambayo inaweza kupelekea vitendo vya Rushwa kutokea na kushauri taasisi husika namna bora ya kurekebisha mapungufu yaliyobainika kwenye chambuzi hizo. Kwa kipindi cha April hadi June 2023, TAKUKURU imefanya chambuzi **7** za mifumo kwenye sekta mbalimbali ikiwa ni pamoja na Ulinzi, vipimo, misitu, maji, miradi ya maendeleo, masoko/biashara na mazingira katika Halmashauri za Mpanda, Mlele na Tanganyika. **(KIAMBATANISHO 2)**

3. TAKUKURU Rafiki

Katika kutekeleza program ya TAKUKURU Rafiki, ofisi ya TAKUKURU kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kutoka kwenye sekta mbalimbali imeweza kushughulikiwa kero **14** kutoka kwenye sekta **7** za Barabara, afya, Ardhi, Utawala, Mapato, Nishati na maji. Aidha, kero hizo zilipokelewa na TAKUKURU kushirikiana na watendaji wa sekta husika kutatua kero zilizolipotiwa na wananchi katika kata zilizopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mlele na Tanganyika.

4. UELIMISHAJI

TAKUKURU imetembelea na kuziimarisha klabu **35** za wapinga Rushwa katika shule za Msingi na Sekondari ambapo kumekuwa na mwamko mkubwa wa vijana katika kupinga Ruhwa na Kukuza maadili ya kitanzania ya kuzingatia haki na usawa.

Vilevile, elimu dhidi ya Rushwa ilitolewa kupitia semina **12** zilizotolewa kwa wafanyakazi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda, wafanyakazi wa taasisi ya umoja wa Amani Kwanza, Kampuni za Ulinzi binafsi,

Wanahabari wa mkoa wa Katavi, Jeshi la polisi (kikosi cha Usalama barabarani), watumishi wa VETA, Wakala wa vipimo (WMA), watumishi wa mifuko ya hifadhi ya jamii na watumishi wa mamlaka ya Viwanja vya ndege.

5. UCHUNGUZI NA MASHITAKA

ofisi ya TAKUKURU imeendelea kupokea malalamiko yanayohusiana na vitendo vya Rushwa.Tumepokea **malalamiko 62,** ambapo taarifa za Rushwa zilikuwa **45** na zisizo za Rushwa **17**. **(KIAMBATANISHO 3)**

Taarifa zinazohusu Rushwa zimeshughulikiwa kwa mujibu wa sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya mwaka 2007 kwa njia ya uelimishaji, uzuiaji pamoja na kuanzisha uchunguzi. Ambapo majalada **6** ya uchunguzi wa wazi (Open Investigation) yalifunguliwa yalitokana na taarifa **45** zilizohusu vitendo vya Rushwa, uchunguzi wa majalada **3** umekamilika huku majalada **4** yakitokana na taarifa zilizopokelewa kwa kipindi cha Aprili-Juni 2023 na mashauri **6** yamefunguliwa mahakamani yaliyotokana na taarifa zilizopokelewa kipindi cha Aprili-Juni 2023 na kufanya kesi zinazoendelea kufikia **12.**

Katika taarifa **17** zisizohusu Rushwa, walalamikaji walishauriwa, ikiwa ni pamoja na kuelekezwa mahali sahihi pa kuwasilisha taarifa zao.

Katika maadhimisho ya wiki ya UTUMISHI WA UMMA kuanzia tarehe 16 Juni 2023 hadi 23 Juni 2023, ofisi ya TAKUKURU mkoa wa Katavi iliadhimisha siku hiyo kwa Mkuu wa TAKUKURU(M) na Naibu Mkuu wa TAKUKURU(M) kwenda kwenye ofisi za TAKUKURU ngazi za wilaya kufanya majukumu yao, ambapo walisimamia utekelezaji wa majukumu ya msingi ya TAKUKURU ikiwa ni pamoja na kupokea malalamiko ya wananchi na kufanya nao vikao vya pamoja ikiwa ni pamoja na kuwaasa watumishi wa TAKUKURU kwenye ofisi hizo kuwa waadilifu na kutojihusiha na vitendo vya Rushwa.

Pia, ofisi ya TAKUKURU mkoa wa Katavi ilitembelea gereza la Mahabusu lililopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda na kutoa misaada yenye jumla ya thamani ya **Tshs. 336,500/=,** ambapo zilitolewa sabuni, miswaki, dawa za meno, Mafuta ya kupaka, vifaa vya kunyolea, nguo za ndani za wanawake na PADS za wanawake.

6. MIKAKATI KWA KIPINDI CHA JULAI – SEPTEMBA 2023

TAKUKURU Mkoa wa Katavi, inatarajia katika robo ya Julai-Septemba, 2023 kuimarisha juhudi za Kuzuia Rushwa kwa kufuatilia na kukagua miradi ya maendeleo na kuhamasisha na kutoa elimu ya ushiriki wa wananchi katika vita dhidi ya Rushwa kupitia nyenzo mbalimbali za uelimishaji ikiwemo vipindi vya Redio pamoja na uelimishaji katika mikusanyiko mbalimbali kwa kutumia mwongozo wa TAKUKURU RAFIKI. TAKUKURU itaendelea kufuatilia kwa karibu fedha zote zinazotolewa na serikali ili kuhakikisha zimetumika kama ilivyokusudiwa na upande wa miradi kuwa bora na thamani ya fedha kuonekana.

Pia tutaendelea kufuatilia makusanyo na uwasilishaji wa mapato yanayotokana na mashine za POS na kuchukua hatua stahiki kwa wale watakaobainika kufuja mali za umma.

Aidha, tutafanya warsha na wadau kujadili matokeo ya chambuzi za mifumo zilizokamilika ili kuweka maazimio ya namna bora ya Kuziba mianya ya ufujaji iliyobainishwa.

Vilevile, kufanya uchunguzi wa haraka kwa taarifa zote zitakazopokelewa na ambazo uchunguzi wake unaendelea.

WITO:

Ndugu Wanahabari,

Mwisho natoa shukurani kwenu Wanahabari kwa ushirikiano wenu mkubwa katika Mapambano dhidi ya Rushwa. Aidha, TAKUKURU Mkoa wa Katavi inatoa wito kwa jamii ya wana-Katavi kwa ujumla kutokujihusisha na vitendo vya kijinai kama kuomba na kupokea rushwa za aina zozote zile.

Hivyo tunatoa rai kwa wananchi wote wa Mkoa wa Katavi kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kwa kupiga simu ya bure 113 na *113# au kutuma ujumbe mfupi wa maneno kupitia namba 113 au kupiga simu ya Mkuu wa TAKUKURU Mkoa ambayo ni **0738-150096** au kufika katika ofisi za TAKUKURU iliyo karibu nawe.

Pia bado kumeendelea kuwa na wimbi la matapeli wanaojifanya ni maafisa wa TAKUKURU ambao hupiga simu kwa watu mbalimbali wakitoa maelekezo na maagizo kwa watu hao ikiwa ni pamoja na kutakiwa kuripoti ofisi fulani ya TAKUKURU au kutaka kuonana na wahusika.

Tunatoa wito na rai kwa jamii na watumishi wote ambao ikitokea wamepigiwa simu na matapeli hao basi wajiridhishe na ofisi ya TAKUKURU iliyoko karibu na maeneo yao au kupiga simu ya bure 113 na *113# au kutuma ujumbe mfupi wa maneno kupitia namba 113 na simu rasmi za TAKUKURU Mkoa wa Katavi ambazo ni 0738150096, 0738150098 (Mlele) na 0738150099 (Tanganyika). Usikubali kutapeliwa, toa taarifa TAKUKURU ili mhalifu huyo aweze kuchukuliwa hatua za kisheria kwani ni kosa la kisheria kujifanya wa TAKUKURU.

"Kuzuia Rushwa ni Jukumu lako na langu, tutekeleze wajibu wetu"

Imetolewana:

Faustine L. Maijo
MKUU WA TAKUKURU (M)
KATAVI.
Simu: 0738-150096